# Sheria zinazolenga makosa ya kingono dhidi ya watoto

Sheria imeimarishwa ili kuongeza ulinzi wa watoto dhidi ya hatari ya unyanyasaji wa kingono.

Sheria mpya zilizoanza tarehe 5 Julai 2021 zinamaanisha:

- watu wazima wote lazima waripoti unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto kwa polisi isipokuwa iwapo wana kisingizio cha kuridhisha
- watu wazima katika mazingira ya taasisi (kwa mfano shule, kanisa au klabu ya michezo) lazima wawalinde watoto dhidi ya hatari ya kosa la kingono linalotekelezwa dhidi yao.

Kwa sheria hizi, *mtoto* inamaanisha mtu mwenye umri wa chini ya miaka 16 au chini ya umri wa miaka 18 na aliye na ulemavu wa akili.

*Ulemavu wa akili*, kama ilivyofafanuliwa katika Kanuni za Jinai, inamaanisha ulemavu unaotokana na ulemavu wa akili, utambuzi au uharibifu wa neva (au mchanganyiko wa haya), ambayo humwacha mtu akiwa na:

- mapunguzo ya uwezo wao wa mawasiliano, mwingiliano wa kijamii au kujifunza
- uhitaji wa msaada.

## Makosa ya kingono dhidi ya watoto

*Makosa ya kingono dhidi ya watoto* ni kosa la tabia ya kingono iliyofanywa dhidi ya mtoto na ni pamoja na:

- Kuchukulia vibaya mtoto
- Kufanya ngono na mtoto au
- Ubakaji
- Ngono ya maharimu
- Kufanya urafiki na mtoto (au mzazi wake au mlezi)
- Kuunda nyenzo za kuwatumia watoto vibaya
- Kudumisha uhusiano wa kimapenzi na mtoto

*Kuwachukulia watoto vibaya* kunashughulikia mienendo mbalimbali ya asili ya kingono. Mifano inaweza kujumuisha:

- kumdanganya mtoto kwa njia ya kingono
- mtoto kugusa sehemu nyeti ya mwili
- kupiga picha ya kingono ya mtoto.

*Kufanya urafiki na mtoto (au mzazi wake au mtunzaji)* inahusu namna baadhi ya wakosaji wanavyofanya mahusiano na kujenga imani na watoto, wazazi, watunzaji, walimu na watoto wengine ili kuwa karibu na mtoto na kujenga fursa ya unyanyasaji wa kingono Inaweza kuwa vigumu kutambua kwa sababu tabia yenyewe inaweza kuwa sio ya unyanyasaji au ya kingono. Unyanyasaji mara nyingi unaweza kutokea kwenye mtandao.

## Kwa nini sheria zinahitajika

Watoto wanahitaji watu wazima walio nao kuchukua hatua za kuwalinda dhidi ya unyanyasaji wa kingono. Makosa mapya yanalenga tabia ambayo inapuuza au kuficha unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto.

### Kushidwa kutoa taarifa

Tume ya Kifalme katika Mwitikio wa Kitaasisi kwa ajili ya Unyanyasaji wa Kingono kwa Watoto (Tume ya Kifalme) iligundua kwamba kushindwa kutoa taarifa za unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto kwa mamlaka husika kuliruhusu kuendelea na kuzuia watoto kupata msaada waliouhitaji.

Idara ya Polisi ya Queensland na Idara ya Watoto, Haki ya Vijana na Masuala ya Tamaduni mbalimbali (Child Safety Services) walitoa taarifa

za unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto. Wamejizatiti kuifanya jamii iwe salama zaidi kwa watoto na kuhakikisha kuwa watoto na vijana wanakuwa salama dhidi ya madhara.

Ili kufanya kazi hii muhimu, huduma hizi zinahitaji watu wazima kuripoti unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto.

Katika tafiti kadhaa za kesi zao, Tume ya Kifalme ilisikia kuhusu mazingira ambayo unyanyasaji haukuripotiwa kwa polisi au ambapo hatua hazikuchukuliwa kuwalinda watoto. Kutoa taarifa ya imani kwamba unyanyasaji wa kingono dhidi ya mtoto umetokea au unatokea kunaruhusu polisi kuchunguza na kukabiliana na makosa ya kingono dhidi ya watoto.

Sheria hizo mpya zinamaanisha watu wazima wote katika jamii wana wajibu wa kisheria wa kutoa taarifa za unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto kwa polisi, isipokuwa wawe na kisingizio cha kuridhisha kwa kutofanya hivyo.

Pata maelezo zaidi kuhusu kushindwa kuripoti makosa.

### Kushindwa kulinda

Sheria mpya pia zinaweka wajibu wa kisheria kwa watu wazima fulani kuwalinda watoto dhidi ya unyanyasaji wa kingono. Watu wazima walio katika nafasi zinazowajibika katika taasisi wana wajibu wa kuwalinda watoto katika utunzaji wao kutokana na hatari kubwa ya unyanyasaji wa kingono.

Kama unajua kuna hatari kubwa ambayo mtu mzima mwingine anayehusishwa na taasisi atamnyanyasa mtoto kingono, haitakiwi kusubiri hadi kosa la kingono litakapotokea ndipo kuwajulisha polisi. Wajibu huu wa kisheria wa kulinda unalenga **kuzuia** unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto

Nia ya sheria hii ni kuhakikisha watu binafsi katika taasisi wanachukua hatua madhubuti za kupunguza au kuondoa hatari zinazojulikana dhidi ya watoto. Sheria inaambatanisha adhabu ya jinai kwa kushindwa kwa kupuuzia au uzembe wa kufanya hivyo.

Pata maelezo zaidi kuhusu kushindwa kulinda makosa.

## Upendeleo

Licha ya vifungu vya kueleza kuhusiana na maungamo ya kidini, makosa hayo hayakusudiwi kubadilisha upendeleo, ikiwa ni pamoja na fursa ya kitaaluma ya kisheria na ushauri wa upendeleo wa kingono.

## Taarifa zaidi

Sheria hizi mpya zinatekeleza mapendekezo kutoka kwa Tume ya Kifalme (Royal Commission) ana ni sehemu ya mfuko mkubwa wa mageuzi ili kuboresha usalama wa watoto na kuwalinda dhidi ya unyanyasaji wa kingono

Soma zaidi kwenye *Sheria ya Makosa ya Jinai (Mageuzi ya Makosa ya Kingono dhidi ya Watoto) na Sheria Nyingine ya Marekebisho ya Sheria ya mwaka 2020*.

Msaada, taarifa na ushauri kwa waathirika unapatikana kutoka:

- Msaada wa Waathirika wa Queensland (Victim Assist Queensland)
- Kids Helpline kwenye 1800 55 1800
- Huduma za Ustawi wa Familia ya Aboriginal na Torres Strait Islander.
- Msaada wa Kisheria Queensland na huduma zingine za kisheria

Tafuta maelezo zaidi kuhusu:

- kuwalinda watoto na kuwasaidia waathirika wa unyanyasaji wa kingono kwa watoto
- ulinzi wa mtoto kutoka Polisi ya Queensland
- unapoweza kuripoti kwenye Huduma za Usalama wa Mtoto.